REPUBLIC OF KENYA

SAMBURU COUNTY GOVERMENT

Samburu County Headquarters
PO Box 3- 20600, Maralal

OFFICE OF THE GOVERNOR

HOTUBA YA MHESHIMIWA MOSES LENOLKULAL GAVANA, KAUNTI YA SAMBURU KWENYE MAADHIMISHO YA SIKUKUU YA MASHUJAA, MARALAL, OKTOBA 20, 2019

Wageni mashuhuri, wananchi kutoka tabaka mbalimbali, mabibi na mabwana,

Hii leo ikiwa ni toleo lingine la maadhimisho ya sikukuu ya mashujaa nchini mwetu, ningependa kuchukua fursa hii kuwakaribisha nyote kwenye awamu hii. Pasingekuwepo ujasiri na ukakamavu wa mashujaa waliojitolea kukomboa Kenya kutoka minyororo ya ukoloni, hatungekuwa na nafasi ya kuisherehekea uhuru tulio nayo kama wananchi wakenya. Ningependa pia kuchukua fursa hii kuwapongeza na kuwajalia heri njema wakenya waliochangia kwa njia moja au nyingine katika uboreshaji na uimarishaji wa maisha kwenye kaunti yetu ya Samburu. Siku hii teule ni awamu muhimu katika kumbukumbu ya historia ya nchi tukufu ya Kenya hivyo imetupasa sote na vizazi vyetu vijavyo kuienzi vilivyo.

Wakenya wenzangu,

Katika miongo iliyopita, historia ya utawala wa Kenya hasa katika enzi za mabepari wa Uingereza, uhuru wa wakenya ulikuwa adimu katika nyanja mbalimbali za kimaisha. Mashujaa waliojitolea mhanga katika ukombozi wa nchi bila shaka ni sababu mojawapo sisi kama wakenya kuimarisha uzalendo wetu.

Mabibi na mabwana,

Utawala wa mfumo mpya wa ugatuzi ni mojawapo ya mabadiliko makuu hasa kwenye sekta ya maendeleo ya umma. Kaunti ya Samburu haijaachwa nyuma kwenye wimbi hili jipya ambalo limebadili hali ya sehemu nyingi nchini Kenya. Serikali ya kaunti ya Samburu kupitia uongozi wangu itaendelea kutilia maanani malengo matatu makuu ya kimaendeleo kwenye sekta za Kilimo, Afya na Elimu. Kwenye sekta ya afya, kaunti ya Samburu imetunukiwa ipasavyo katika kutumia ugatuzi kama nafasi mwafaka wa kutatua baadhi ya changamoto za afya zinazowakumba wakaazi humu. Nchini Kenya, kwenye miaka tangulizi, utafiti na takwimu zilionyesha hali duni ya afya katika kaunti ya Samburu. Kupitia ugatuzi, serikali ya kaunti ya Samburu hata hivyo imeweza kudhibiti hali hiyo kwa kuzingatia afya ya akinamama na watoto hivyo kupunguza visa vya vifo vinavyotokana na hali duni ya afya. Kwenye juhudi za kupunguza mzigo wa magonjwa, vituo vya

afya vimeweza kuongezeka kwenye maeneo yetu ya mashinani, la muhimu ikiwa ni maeneo yaliyosahaulika kwa muda na yaliyokumbwa na changamoto za kutopata huduma za afya. Vilevile, idara ya afya ya kaunti ya Samburu imeweza kununua ambulensi kumi na mbili miaka minne iliyopita ambazo zimesaidia pakubwa kuokoa maisha hasa kwenye hali ya kidharura. Mwezi Juni mwaka huu kaunti ya Samburu ilipokea kutoka Benki ya dunia ambulensi moja na gari la kubeba dawa. Kadhalika, tumeweza kuwafikia watoto zaidi kwenye maeneo yetu ya mashinani kwa kuwachanja dhidi ya magonjwa. Serikali ya kaunti kupitia idara ya afya pia imeweza kuanzisha kitengo cha matibabu ya magonjwa ya figo na kuongeza vyumba vinne vya upasuaji vya kisasa pamoja na maabara mawili. Hatua hizi pamoja na mengine zitapelekea katika kuwezesha utoaji wa huduma kwenye vituo vipya vya afya kupitia ajira ya wafanyikazi zaidi wa afya, utoaji wa mafunzo maalum kwa wafanyikazi wetu wa afya, kuwapa motisha na kuimarisha uhusiano zaidi na washikadau katika sekta ya afya.

Ndugu zangu,

Kama tujuavyo, kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu na nguzo ya lishe bora kwa jamii zetu. Japo maeneo mengi, katika kaunti hii yapo kwenye sehemu kame, hali hii haijakuwa kikwazo kwenye juhudi za uimarishaji wa kilimo. Uwepo wa usalama wa lishe kwa jamii ni mojawapo

ya ajenda muhimu katika serikali ya kaunti. Idara ya kilimo ya serikali ya kaunti itaendelea kubuni mikakati ya kuimarisha kilimo katika kaunti ndogo za Samburu ya kati, mashariki na kaskazini. Wakulima katika maeneo mbalimbali kwenye sehemu za Samburu mashariki, kaskazini na kati tayari wamenufaika na miradi ya utoaji wa mbegu, mbolea na ngamia. Msimu huu wa mvua unapoendelea kushuhudiwa kwenye maeneo tofauti katika kaunti ya Samburu, imewapasa wakulima wetu walioko nyanda za juu kutia juhudi katika uimarishaji wa kilimo ndogo ndogo japo msimu huu wa mvua utachukua muda mfupi. Idara ya kilimo ya serikali ya kaunti pia imeimarisha uhusiano na washikadau kutoka serikali kuu kupitia mradi wa kitaifa ya ukuaji wa kilimo sehemu za mashambani, al maarufu NARIGP. Wakulima wameweza kupokea mafunzo maalum yanayohusiana na kilimo bora, vilevile msaada wa kifedha wa kuendeleza kilimo biashara, uimarishaji wa soko za mifugo pamoja na maendeleo mengine.

Wananchi wenzangu,

Ukosefu wa elimu mwafaka katika kaunti ya Samburu si jambo geni ikiwa ni mojawapo ya vigezo vilivyochangia uwepo wa hali duni ya maendeleo katika baadhi ya sehemu za kaunti hii. Mfumo wa ugatuzi umechangia pakubwa usajili mkubwa wa watoto wetu katika shule za chekechea hivyo kuinua asilimia ya wanaojiunga na shule za misingi ikilinganishwa na miaka za

awali. Tuwasajili watoto kwenye shule za chekechea zinazotoa elimu ya bure ndiposa tupate kuimarisha masomo ya msingi vilivyo. Kufikia sasa serikali ya kaunti kupitia idara ya elimu imeweza kujenga na kufadhili zaidi ya vituo mia tatu vya utoaji wa masomo ya chekechea kwa watoto wetu. Mnamo mwezi Juni mwaka huu, idara ya elimu ilitoa ajira kwa walimu sitini na kuwatuma sehemu mbalimbali katika kaunti ili kutoa masomo kwa watoto wetu. Kufikia sasa, serikali ya kaunti ya Samburu imeweza kuajiri waalimu mia sita na saba tangu miaka za uanzilishi wa ugatuzi. Miaka ya awali, hali ya elimu ya chekechea ilikuwa duni mno katika kaunti hii lakini mabadiliko yaliyoshuhudiwa kupitia ugatuzi zimepiga hatua katika kubadili hali hiyo pakubwa. Mapema mwaka huu kaunti ya Samburu ilipeana jumla ya shilingi milioni sitini na tano pesa za karo na usomi Al maarufu Bursary and Scholarships. Mradi huu wa pesa za karo na usomi utaendelea kila mwaka.

Vilevile, idara ya barabara na uchukuzi inawania kufungua barabara zaidi kwenye sehemu tofauti katika kaunti ya Samburu. Kufikia sasa, jumla ya kilomita mia sita na tisini za barabara mipya zimeweza kufunguliwa na serikali ya kaunti tangu ugatuzi. Mradi wa mwangaza kwa miji yetu pia utaendelea. Huduma hii kwa sasa ikitumiwa na wakaazi wa miji ya Maralal na Baragoi. Mji wa Wamba pia utanufaika na mradi wa mwangaza. Kaunti ya Samburu pia imebuni bodi la manispaa ya Maralal. Huduma tofauti zitaboreshwa hivi karibuni katika manispaa ya Maralal baada ya ubunifu wa

bodi na uajiri wa meneja wa manispaa. Katika juhudi za kuimarisha umiliki wa ardhi idara ya ardhi kaunti ya Samburu itaendelea na miradi ya utoaji wa hati miliki kwa mashamba ya kijamii yaani Group ranches ambayo hayajapokea hati hizo. Baadhi ya mashamba ya kijamii pia yameweza kunufaika na miradi ya ukataji wa ardhi hivyo kuwezesha wakaazi kuwa na umiliki wa kibinafsi wa ardhi zao. Shughuli za upangaji wa miji yetu pia inaendelea hivyo kutuwezesha kutoa huduma za umma vilivyo. Mojawapo ya hatua nyingine tuliyoweza kutekeleza katika idara ya ardhi ya serikali ya kaunti pamoja na shirika la FAO ni kuwa na maabara iliyo na mitambo ya kisasa yatakayotumika kutatua na kutekeleza maswala kadha wa kadha yanayohusiana na ardhi. Vilevile, sajili ya ardhi itaweza kuletwa kwenye makao makuu ya kaunti mjini Maralal hivyo kuwezesha wananchi kupokea huduma zinazohusiana na ardhi kwa karibu kinyume na kusafiri hadi mjini Nyahururu jinsi ilivyo sasa. Maabara na sajili ya ardhi yatapatikana kwenye afisi zetu za kaunti hapa mjini maralal. Kama nilivyowahidi, jengo la makao makuu ya kaunti limekamilika na linatumika na maafisa wa kaunti kuboresha huduma kwa wananchi. Wananchi sasa wanaweza kupata huduma kwenye jengo moja kinyume na awali.

Wakenya wenzangu,

Kwenye miaka ya kifedha ya elfu mbili kumi na saba na kumi na nane pamoja na mwaka huu wa kifedha, serikali za kaunti nchini Kenya zilikumbwa na changamoto za utoaji wa fedha za kimaendeleo kutoka hazina ya kifedha ya kitaifa. Kaunti ya Samburu vilevile iliathirika pakubwa kwenye changamoto hiyo. Hali hiyo ilipelekea miradi mingi ya kimaendeleo kutokamilishwa na wanakandarasi. Ni makadirio yangu kuwa miradi ya kimaendeleo iliyokwama na iliyoanzishwa na serikali ya kaunti itaendelea na kukamilishwa kwa wakati ufaao.

Hivi majuzi kumekuwa na visa vya vurugu na taharuki kutokana na mauaji yaliyosababishwa na wezi wa mifugo kwenye eneo la Samburu kaskazini. Ningependa kuwasihi wakaazi wa maeneo hayo kudumisha amani miongoni mwao. Wengi wamepoteza maisha kutokana na vita hivyo vya mara kwa mara. Hali hiyo pia imepelekea kuzorota kwa viwango vya uchumi na elimu kwenye sehemu zilizoathirika na vita hivyo. Kadhalika ningependa kuwarai vikosi vya kiusalama kuongeza juhudi zaidi katika kupambana na wezi wa mifugo wanaozidi kuwahangaisha wakaazi katika maeneo hayo. Zaidi ya hayo naomba wizara husika kurejesha bunduki ya askari wa akiba haraka iwesekanavyo baada ya usajili kwani walisaidia pakubwa kupambana wa wezi wa mifugo.

Wananchi watukufu,

Ningependa vilevile kushukuru bunge letu la kaunti ya Samburu. Pasingekuwepo ushirikiano dhabiti kati ya vitengo viwili vya serikali ya kaunti yetu, basi hatungeweza kuendesha baadhi ya shughuli na huduma serikalini. Uongozi wangu utatilia maanani swala la uadilifu katika utoaji wa huduma za umma. Kwa haya na mengine, asanteni na Mungu awabariki.